**Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia**
*Aliishi Yerusalemu. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Kisha aliishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Akawa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.*

**Gazeti la Parokia Katoliki ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran**
*N. 81 — Mwaka wa 13*
**Machi 2021**

# SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO

*Kwaresima na Pasaka 2021*

## Kumbuka Mungu na wenzako

Baada ya miezi kadhaa, Gazeti letu latolewa tena. Mwaka uliopita lilisimamishwa baada ya kufunga Makanisa kwa sababu ya janga la Corona. Wakati huu, kazi na shughuli nyingi za Kanisa zimerudi, na hata Sauti ya Mtakatifu Marko yastahili kusikika tena.

> Toba ni kujisahau kiasi, Sala ni kumkumbuka Mungu, Huruma ni kuwakumbuka wenzetu.

KWARESIMA na PASAKA - Mwaka uliopita hatukuweza kufanya Paska pamoja: ulikuwa wakati wa kufunga Makanisa. Lazima mwaka huu tuadhimishe vizuri sikukuu za Paska, yaani siku za Mateso, Kifo na Ufufuko wa Bwana Yesu Kristu. Kipindi cha Kwaresima, tulichoanza Jumatano ya Majivu, ni wakati unaofaa kwa kujitayarisha. Tunaweza kufanya nini ili tuwe tayari? Kwaresima inatukumbusha mambo matatu ya kufanya wakati huu, yaani: Toba, Sala na Huruma.

TOBA: ni **kujisahau kiasi**, kuacha kujijali kupita kiasi, kutupa majivuno na ubinafsi, kujinyima anasa, kutubu dhambi, kufanya kitubio, kubadilisha mawazo, kurekebisha tabia. Yaani, duniani humu siko peke yangu wala si mimi na mahitaji yangu jambo la kwanza la kushughulikia. Kunao wengine ambao nafaa kuwajali zaidi yangu mwenyewe: ndio Mungu na wenzangu.

SALA: hiyo ni **kumkumbuka Mungu**, kusali zaidi, kusikia Neno lake, kuongeza imani kwake, hadi kufanya mapenzi yake.

HURUMA: ni **kuwakumbuka wengine**, yaani wenzangu, majirani, wenye shida, kusaidiana nao, na kurudisha haki katika jamii.

Kama tungekubali kuishi hivyo! Maisha yetu yangekuwa afadhali sana. Hivyo Paska itakuwa kwa kweli sherehe ya upatanisho!

Tuendelee pia kuiombea dunia nzima, hasa wanaoteseka kwa sababu ya Corona, tena waliokufa: Mungu atusaidie sote kusaidiana katika changamoto, na kumtambua yeye mwenye uwezo wote.

Fr. Giacomo Basso - *Baba Paroko*

*Ibada ya Jumatano ya Majivu Ol Moran, tarehe 17 Februari, mwanzo wa Kwaresima.*



### KWARESIMA NA MWEZI WA TATU

*Kanisa liliingia katika Kipindi cha Kwaresima* ***Jumatano ya Majivu****, tarehe 17 Februari.* ***Kwaresima****, maana yake siku arobaini, ni wakati wa toba na maandalizi ya kiroho kwa ajili ya Sherehe Kuu ya Pasaka ya Mateso, Kifo na Ufufuko wa Bwana. Pia, ni wakati wa pekee wa kutayarisha Wakatekumeni kwa Ubatizo.* ***Juma Kuu*** *litaanza Jumapili ya* ***Matawi****, tarehe 28 Machi, Jumapili ya* ***Pasaka*** *itakuwa tarehe 4 Aprili.*

*Mwezi wa tatu, Kanisa huadhimisha pia sherehe mbili muhimu. Tarehe* ***19 Machi*** *ni Sherehe ya Mt. Yosefu, Mume wa Bikira Maria, Mlezi wa Mtoto Yesu, Msimamizi wa Kanisa lote. Tarehe* ***25 Machi****, miezi tisa kabla ya Yesu kuzaliwa, ni sherehe ya Maria kupashwa habari na Malaika kuwa Mama wa Mkombozi (Annunciation of the Lord), Maria alipopata mimba ya Yesu, mwanzo wa Mwana wa Mungu kutwaa mwili wa kibinadamu.*

*Maombi ya Ijumaa ya Kwaresima*

### NJIA YA MSALABA MAKANISANI

*Maombi ya Njia ya Msalaba husaidia kukumbuka mateso ya Kristu, na kuwaombea Wakristu na watu wote wokovu. Maombi haya hufanywa kila Ijumaa ya Kwaresima katika Makanisa Madogo. Nayo ni nafasi ya pekee ya kuongeza bidii katika sala.*

*Mapadri pia huongoza* ***Njia ya Msalaba*** *kila Ijumaa, 3pm, Ol Moran. Tena, katika Makanisa Madogo, pamoja na* ***Sakramenti ya Kitubio****, kuanzia 02.00pm, - 19 Februari: Githima; - 26 Februari: Miharati; - 5 Machi: Kabati; - 12 Machi: Survey; - 19 Machi: Mithuri; - 26 Machi: Kahuho.*

*Kisha, Ijumaa Kuu ya Mateso, tarehe 2 Aprili, Njia ya Msalaba itafanywa 10am: Magadi (Mt. Mikaeli Zone); 3pm: Minjore (Mt. Maria Goretti Zone); 3pm: Ol Moran (Mt. Karolo Lwanga Zone).*

*Kitabu cha Njia ya Msalaba:* ***KShs 100/=***



*Juu:* Viongozi wa Parokia nzima katika Parish Assembly ya 15, Ol Moran, Jumamosi 13 Februari.

*Parish Baraka Day itakuwa Jumapili 25 Aprili*

# 15th Parish Assembly

*Viongozi wa Parokia nzima walikutana katika Parish Assembly ya 15, Jumamosi 13 Februari, ili kupanga kazi za mwaka huu. Wakajadiliana kuhusu mambo kadhaa yanayohusu maisha ya Parokia:*

*1) Hali na changamoto ya maisha ya Kikristu ya watoto na vijana wa Parokia (**PMC** na **Youth**), na Registration yao kwa mwaka 2021.*

*2) Makanisa mapya na uteuzi wa **Makatekista**, pia haja ya kutafuta Makatekista wapya, na kuwafunza.*

*3) **Parish Baraka Day**, itakayofanywa Jumapili 25 Aprili, Sherehe ya Mt. Marko Mwinjili, Msimamizi wa Parokia. Sadaka zake zitasaidia miradi ya Parokia.*

*4) **Utaratibu wa mwaka** huu wa kazi za Parokia, vikundi na vyama, pia sherehe ya mwaka ujao kwa ajili ya miaka 25 ya Parokia.*

*5) Ripoti ya michango, zaka na sadaka ya mwaka 2020, pia mpango wa **michango ya mwaka 2021** kwa ajili ya Jimbo la Nyahururu.*

*Mapadri wa Parokia*

# Fr. Peter na Fr. Simon

Mwishoni mwa mwaka uliopita kulikuwa na mabadiliko ya Mapadri kwenye Parokia yetu. Baba Askofu Joseph alimteua Fr. Peter Kinyua kuwa Baba Paroko wa Parokia ya Mtakatifu Yosefu Mfanyakazi ya Mochongoi, pia akamtuma kwetu kama Padri Msaidizi Fr. Simon Ngatia. Fr. Peter, baada ya kuhudumu hapa Ol Moran kwa muda ya miaka mitatu, aliingia Parokia ya Mochongoi tarehe 4 Desemba. Baadaye, Jumapili 17 Januari, alialikwa tena kwetu kuongoza Misa ya shukrani na ya kuagana na Wakristu. Katika ibada hiyo tulimpokea Fr. Simon pia.





*Kushoto:* Fr. Peter alipokelewa na Viongozi wa Mochongoi baada ya kuagana na Wakristu wa Ol Moran, Jumapili 17 Januari.

*Kulia:* Fr. Peter na Fr. Simon

**Fr. Peter Ndumu Kinyua** *alizaliwa mwaka 1986, ametoka Igwamiti. Alipadrishwa mwaka 2017, akateuliwa Padri Msaidizi wa Ol Moran. Tarehe 30 Novemba 2020 aliteuliwa kuwa Baba Paroko wa Parokia ya Mochongoi.*

**Fr. Simon Muriithi Ngatia** *alizaliwa mwaka 1987, ametoka Muhotetu. Alipadrishwa mwaka 2019, akahudumia katika Parokia za Ngano na Ndunyu Njeru. Tarehe 30 Novemba 2020 aliteuliwa kuwa Padri Msaidizi katika Parokia yetu ya Ol Moran.*

*Nakwam, Posta, Naibor, Ngoisusu*

# Injili vijijini

Parokia inaendelea kupanuka katika vijiji vipya vinavyolingoja Neno la Injili. Ni kazi kubwa iliyo mbele yetu: tunahitaji hasa Makatekista wapya wanaoshiriki katika huduma na uenezaji wa Injili.

NAKWAM - Kijijini Nakwam, kupita Lounyek kuelekea Baringo, Wakristu kadhaa wameendelea kukutana Jumapili kwa ajili ya maombi. Makatekista wameshaanza kuwashughulikia, pia Mapadri wameanza kuwafanyia ibada ya Misa mara inapowezekana.

POSTA - Wakristu hukutana shuleni kwa ajili ya ibada, lakini mwezi uliopita Kanisa limepewa ploti katika kijiji cha Posta, ili liweze kuitumia kwa ajili ya huduma ya Wakristu.

NAIBOR - Tena, katika kijiji cha Naibor, baada ya kupita Posta kuelekea Sukuta, Parokia imepewa sehemu ya shamba kwa ajili ya Kanisa, karibu na shule mpya ya Naibor.

NGOISUSU - Kuna matayarisho ya kufungua tena Kanisa kijijini Ngoisusu, kati ya Ol Motunyi na Posta. Wenyeji waliomba Parokia iwasaidie kikanisa, wakajitolea kujenga nyumba kwenye shamba la Kanisa huko, kwa ajili ya shule ya watoto wadogo na pia kwa ajili ya ibada ya Jumapili.

*Chini:* Mapadri na viongozi kwenye mkutano Ngoisusu



*Small Christian Communities*

# Ziara ya Jumuiya

Mwezi wa kwanza, Fr. Simon alianza ziara ya kuwatembelea Wakristu katika Jumuiya Ndogo Ndogo za kila Kanisa Dogo la Parokia. Kwa kweli, familia na Jumuiya Ndogo Ndogo ni vituo vya kwanza vya maisha ya Kanisa.

Katika ziara yake, Padri hutoa ibada ya Misa, kuwapatia Wakristu Sakramenti ya Kitubio, mafunzo ya Kikristu, na kuwatembelea wagonjwa wa jumuiya.

Fr. Simon alianza ziara kule Gituamba na Minjore, sasa anaendelea katika Kanisa la Miharati. Baadaye, atatembelea Kabati, Ol Moran, kisha katika Makanisa mengine mpaka kuzifikia Jumuiya zote.

*Shule ya Parokia itakuwa “Day & Boarding”*

# Mabweni ya Tumaini

MABWENI MAPYA - Mradi wa kujenga mabweni mapya umeendelea katika Tumaini Academy, shule ya msingi ya Parokia. Kazi ilianza mwezi wa saba 2020 kwa ajili ya bweni la wasichana. Mjengo utatumiwa kuanzia mwezi wa tano. Mpango ni kujenga pia bweni la wavulana na chumba kikuu cha mamkuli. Ombi la kufanya shule ya Parokia itambuliwe na Serikali kama *‘Mixed Day & Boarding School’* imeshapelekwa katika Ofisi ya Elimu ya Serikali ya Laikipia County. Baadaye, huduma ya mabweni itakuwa *Schooling Children Rescue Centre* pia. Tumaini Academy itakuwa shule ya kwanza kupeana hiyo huduma katika eneo letu. Mchoraji wa hiyo mijengo ni Arch. Stefano Battaglia (Venisi, Italia), na kampuni ya ujenzi ni Jonju Building Contractors, ya Eng. Joseph Njuguna (Nyahururu).

MAJI - Pamoja na hayo, shule imekamilisha kazi ya kupeleka maji kwa mijengo ya shule, pia kutengeneza kioski la maji nje ya shule kwa ajili ya majirani.

MWALIMU MKUU - Mwaka huu ulianza na mabadiliko katika uongozi wa shule pia. Mwalimu Jacob Ng’etich aliteuliwa kuwa Mwalimu Mkuu, baada ya mwalimu John Wanyama kuajiriwa na TSC. Pia mwalimu Teresia Ng’ang’a aliteuliwa kuwa naibu wa Mwalimu Mkuu.

KCPE - Shule ilifungua tena mwezi wa kwanza. Wanafunzi 40 wa darasa la nane, wasichana 22 na wavulana 18, wanajiandaa kwa mtihani wa KCPE.



*Juu:* Mjengo wa mabweni mapya ya Tumaini Academy.

*Chini:* Kituo cha maji ya Tumaini; Wanafunzi wa shule ya Parokia; Admin. bw. Muthua, Mwalimu Wanyama, H/T mpya Jacob, na D.H/T Teresia.








*Bidii ya Laikipia North CDF*

# Maendeleo katika Shule za Eneo

Bidii kwa ajili ya maendeleo ya shule inaendelea kuonekana katika eneo la Laikipia North. Kwa njia ya CDF, Shule za Msingi na za Upili zimeweza kupata misaada mbalimbali, hasa kwa ajili ya mijengo ya madarasa mapya. Lakini, miradi miwili imekuwa na matokeo ya kipekee:

BUS YA MITHURI - Shule ya Upili ya Mithuri imeweza kupokea Bus mpya. Mheshimiwa Sara Lekorere, MP Laikipia North, alikuja mwenyewe kuikabidhi kwa shule Ijumaa 22 Januari.

NAIBOR AMANI PRIMARY - Mradi mwingine wa maana sana unaendelea katika kijiji cha Naibor. Jumapili 21 Februari Baba Paroko alialikwa kutoa ibada ya Misa ya Shukrani na kuibariki shule mpya ya msingi, inayoitwa Naibor Amani Primary. Shule hii inaenedelea kujengwa na CDF pamoja na ufadhili wa Loisaba Conservancy. Sherehe ilihudhuriwa na MP Sara, Mheshimiwa Francis Ole Kaparo, bw. Tom Silvester, CEO wa Loisaba Conservancy, pamoja na wanafunzi na watoto wa shule, na watu wengi wa jamii za eneo. Wanafunzi wa Ol Moran High School, Hekima House, Tumaini Academy na Laikipia North Technical & Vocational College (Posta) walisaidia kuongoza nyimbo za ibada. Baada ya baraka, iliyoandamana na mvua nzuri ya siku hiyo, waakilishi wa jamii mbalimbali walicheza pia nyimbo za kitamaduni.





*Juu:* Baraka ya Shule ya Naibor Amani, pamoja na MP Sara Lekorere.

*Chini:* Bus ya Mithuri Sec. inakabidhiwa.






### *Suala la Kijamii: Mbona hii Fujo yote kwetu?*

*Nini inaendelea katika jamii siku hizi? Fujo na unyama zimezidi. Tumeona mambo katika eneo letu: juma lililopita mzee Gabriel Macharia aliuawa usiku akiwa nyumbani kwake Kahuho; juzi tena kijana Daniel Loseku alipigwa na wenyeji wa Bondeni, akafa; Januari askari Simon Kimayo aliuwawa Wangwachi na wafugaji haramu. Lakini si uuaji tu: mwaka uliopita mtoto mlemavu Charity, Kahuho, alinajisiwa na kupewa mimba; mtoto Sheila, Githima, aildhulumiwa na kuvunjwa baadhi ya sehemu za mwili. Hizo kesi zilifika mpaka kwa mitandao. Zaidi ya hayo, kiasi gani cha fujo kimejificha katika vijiji vyetu? Mzee kuchapa bibi yake; mwalimu kuchapa mtoto; serikali kuchapa wafungwa au raia. Mwanaume kumharibu msichana, mpaka mtoto au mlemavu! Mara nyingi ripoti haipigwi, tunaogopa kulinda haki za watu na kusema ile fujo tunayoona, ama tunaimaliza kienyeji. Wapi heshima kwa watu na thamani ya uhai? Fujo hii yote imesababishwa na nini? Kwa nini kutumia sheria ya nguvu, kuliko nguvu ya sheria?*

HABARI FUPI

## Makatekista

Mpango wa kuwafunza Makatekista Wapya (ama Junior Catechists) utaanza tena hivi karibuni. Parokia inahitaji Wakristu walio tayari kujitolea kwa ajili ya huduma ya Ukatekista katika Makanisa Madogo, pia katika Makanisa mapya. Viongozi pia wanaombwa kuwatafuta Wakristu wanaostahili kwa huduma hiyo.

## PMC

Watoto na Promoters wa PMC wanaendelea kujiandikisha kwa mwaka huu, na kupanga kazi zao. Jumapili 17 Januari watoto kutoka kila Kanisa walifanya Nadhiri za mwaka katika ibada iliyoongozwa na Fr. Peter Kinyua. Mwezi wa Februari walipata nafasi za masomo ya pekee katika kila zone kuhusu maisha ya Kikristu. Wakati huu pia wanaendelea kujitayarisha katika Zones kwa mashindano ya nyimbo. Viongozi wa PPC waliamua pia kwamba mwaka huu kutakuwa na PMC Baraka Day kwa kuchangia miradi ya watoto wetu: itafanywa Ol Moran, Jumapili 6 Juni, baada ya maandamano ya Sherehe ya Mwili na Damu ya Kristu.

## Vijana

Vijana wa Parokia wanaendelea kufanya *Registration 2021* kwa Jimbo la Nyahururu. Viongozi watano kutoka kila Kanisa Dogo walikutana katika Halmashauri ya Vijana Jumamosi 27 Februari, pamoja na Patrons na Matrons wao, kwa kupanga kazi za mwaka huu.

Jumamosi 27 Machi, waliojiandikisha watakuwa na sherehe jioni: *'Youth Barakoa Party!'*. Kesho yake, 28 Machi, watafanya Nadhiri zao katika Misa ya Jumapili ya Matawi. Kisha, kuanzia Alhamisi Kuu 1 Aprili hadi Jumapili ya Pasaka 4 Aprili, watakuwa na Semina ya Pasaka (*Easter Seminar*), kwa kuadhimisha pamoja ibada za Pasaka.

Jumapili 11 Aprili, vijana wote wa Jimbo walialikwa katika Misa ya Baba Askofu, kule Tabor Hill. Shati rasmi ya Vijana wa Jimbo imetengenezwa pia, na inaendelea kununuliwa na waliojiandikisha.

Hata Vijana wa Parokia watakuwa na *Youth Baraka Day* mwaka huu, kwa kuwashikilia katika miradi yao, Jumapili 15 Agosti, Ol Moran.

## Choir

Wanakwaya wataanza hivi karibuni semina za nyimbo katika Parokia na kutjitayarisha kwa mashindano. Pia, wanajiandaa kwa nyimbo za ibada ya Juma Kuu na Pasaka.

## Vyama

**CA** - Jumamosi 21 Machi kutakuwa na safari ya kidini ya wanachama wote wa Ng'arua Deanery kwenda Nanyuki. Mkutano wa wanachama wote utakuwa Jumatano 1 Aprili.

**CMA** & **CWA** - Hata mwaka huu, wanachama wa CMA na CWA watafanya Nadhiri zao siku ya sherehe ya Parokia, Jumapili 25 Aprili, katika ibada ya Parish Baraka Day. Akina baba na mama wanaendelea kujiandikisha na kupanga shughuli za mwaka.

**CMA** - Jumatano 10 Machi kutakuwa na mkutano wa viongozi wa CMA wa kila Kaniisa Dogo, Ol Moran 10am. Wanachama wote wa Jimbo watakuwa na siku ya maombi kule Subukia Jumamosi 1 Mei, sherehe ya Mt. Yosefu Mfanyakazi.

**CWA** - Mwezi uliopita wanachama wa CWA walikuwa na Semina katika Zones ili kujitayarisha kwa nadhiri za mwezi wa nne.

## Scouts

Hata Maskauti wa Parokia walianza tena kazi zao. Viongozi walikutana kupanga shughuli za kila sehemu ya chama, yaani Sungura, Chipukizi, Mwamba na Rovers. Jumamosi 6 Mwamba na Rovers watakuwa na Hike kule Ol Motunyi, kwa ajili ya 'Pass Out Ceremony' ya wanachama wa kidato cha nne watakaotoka Mwamba na kuingia Rovers.

Kutakuwa pia na masomo ya PTC (Primary Training Course) kwa ajili ya Viongozi wa Chama wa Sub-County, kuanzia Jumatatu 12 Aprili, shuleni kwetu Tumaini Academy.

## Jimbo la Nyahururu

- **Jimbo la Nyahururu latimiza miaka 18** Alhamisi 25 Machi, Sherehe ya Maria Kupashwa Habari (Annunciation).
- **Sadaka Maalum ya Kwaresima:** Katika kila Parokia ya Jimbo, sadaka za Misa za kila Jumapili ya Kwaresima ni Sadaka Maalum kwa ajili ya maskini na wasiojiweza.
- **Michango 2021** ya kusimamia Jimbo na miradi yake ishaanza katika kila Parokia.

### Utaratibu wa Machi-Aprili 2021

*Jumapili 7 Machi* - ya 3 ya Kwaresima *(Yoh 2:13-25)*
→ Misa - 8am: Ol Motunyi; 9am: Lounyek; 10.30am: Dam Mbili; 11am: Ol Moran; 12noon: Ndunyuriwo; 3pm: Ol Moran

*Ijumaa 12 Machi*
→ 2.00pm: Survey, Kitubio na Njia ya Msalaba pamoja na Padri
→ 3.00pm: Ol Moran, Njia ya Msalaba

*Jumapili 14 Machi* - ya 4 ya Kwaresima *(Yoh 3:14-21)*
→ Misa - 8am: Minjore; 9am: Magadi; 10am: Mithuri; 11am: Ol Moran; 12noon: Mbombo; 3pm: Ol Moran

*Ijumaa 19 Machi* - Sherehe ya Mt. Yosefu, Mume wa Bikira Maria
→ 7.00am: Ol Moran, Misa ya Sherehe
→ 2.00pm: Mithuri, Kitubio na Njia ya Msalaba pamoja na Padri
→ 3.00pm: Ol Moran, Njia ya Msalaba

*Jumapili 21 Machi* - ya 5 ya Kwaresima *(Yoh 12:20-33)*
→ Misa - 9am: Kahuho, Survey; 11am: Posta, Ol Moran
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni

*Alhamisi 25 Machi* - Sherehe ya Maria Kupashwa Habari ya Kuzaliwa Bwana Yesu Kristu *(Annunciation of the Lord)* (Lk 1:26-38)
*- Sherehe ya Miaka 18 ya Jimbo*
→ 7.00am: Ol Moran, Misa ya Sherehe

*Ijumaa 26 Machi*
→ 2.00pm: Kahuho, Kitubio na Njia ya Msalaba pamoja na Padri
→ 3.00pm: Ol Moran, Njia ya Msalaba

*Jumapili 28 Machi* - **Jumapili ya Matawi** *(Mk 11:1-10)*
*Mwanzo wa Juma Kuu*
*(tazama Utaratibu wa Ibada za Juma Kuu 2021 katika The Echo)*

*Alhamisi Kuu - 1 Aprili* - Karamu ya Mwisho wa Bwana

*Ijumaa Kuu - 2 Aprili* - Mateso na Kifo cha Bwana wetu Yesu Kristu

*Jumamosi Kuu - 3 Aprili* - Kesha ya Pasaka

*Jumapili 4 Aprili* - **PASAKA ya Ufufuko** *(Yoh 20:1-9)*
→ Misa - 9am: Magadi, Lounyek; 10.30am: Dam Mbili; 11am: Ol Moran; 12noon: Ndunyuriwo
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni

*Jumapili 11 Aprili* - Jumapili ya 2 ya Pasaka *(Yoh 20:19-31)*
→ Misa - 7am: Ol Motunyi; 8am: Minjore; 9am: Kahuho; 10am: Mithuri; 11am: Ol Moran; 12noon: Mbombo
→ 9am: Nyahururu, Misa ya Askofu pamoja na Vijana wa Jimbo

*Jumamosi 17 Aprili*
→ 10am: Ol Moran, Misa ya Nadhiri za Masista Wapya

*Jumapili 18 Aprili* - Jumapili ya 3 ya Pasaka *(Lk 24:35-48)*
→ Misa -8am: Gituamba; 9am:Survey; 10am: Posta; 11am: Ol Moran

*Jumapili 25 Aprili* - Jumapili ya 4 ya PASAKA *(Yoh 10:11-18)*
**Sherehe ya Mtakatifu Marko Mwinjili**, Msimamizi wa Parokia
PARISH BARAKA DAY
→ 10am: Ol Moran, Misa Kuu ya Sherehe (Wakristu wote)

SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO
- No. 81, Year 13, Printed on 1th March 2021 - (NOT FOR SALE)
**SAINT MARK** CATHOLIC PARISH - Ol Moran - *Catholic Diocese of Nyahururu*
*P.O.Box 20 - 20320 Kinamba* - saintmark@olmoran.it - *+254 720 924 153*